

Muhtasari wa maelezo

Athari za janga la COVID-19 kwa wakimbizi na ulinzi wao nchini Kenya, Uganda, Ghana, Nigeria, Afrika Kusini na Zimbabwe

Janga la sasa la COVID-19 linaathiri watu wote kote ulimwenguni lakini wale walio katika nafasi za hatari, ikiwemo wakimbizi na watu waliohamishwa, wanaweza kuwa katika hatari zaidi. Katika somo la karibuni, tuliangalia ambavyo janga la COVID-19 liliathiri wakimbizi na ulinzi wa kikimbizi katika nchi sita katika Afrika Magharibi, Afrika Mashariki na Afrika Kusini, kwa majina Ghana, Kenya, Nigeria, Afrika Kusini, Uganda, na Zimbabwe, katika mwaka wa kwanza wa janga na mpaka pia February 2021. Kwa kutumia dodoso lisilio la uwakilishi, tulitaka kupata yaliomo ndani katika mitazamo ya watu walio na mandhari nyuma ya kikimbizi, wasomi, wafanyakazi wa serekali na watendaji wa misaada wanaofanya na au kwa wakimbizi. Jumla ya 90 waliohojiwa walijaza dodoso.

Kutokana na majibu, ni ushuhuda ya kuwa hali ya wakimbizi na watu waliohamishwa kujikuta wenyeji katika nchi waliyokimbilia tayari ilikuwa ni changamoto kabla ya janga. COVID-19 imeongeza changamoto hizi, kwa sehemu na pia imetengeza hatari mpya. **Washiriki walisitiza ya kuwa ugumu wa uchumi, mipaka ya kipato na uchache wa huduma, afya na hatari za usalama ni miongoni mwa changamoto kubwa zilijitokeza** kutokana na janga.

Japokua maendeleo katika nchi na majibu ya serikali kwa janga yalitofautiana, washiriki waliangazia athari sawa. **Vitendo vya serikali kama vile kufungwa kwa mipaka au kuwekwa kwa lockdown zilikuja na athari kali kwa wakimbizi na wanaotafuta hifadhi, kuwaacha wakikwama, kuwafanyia vigumu kwa kupata huduma ya afya na huduma nyingine au kutoka kwa ajili ya kutafuta**

mapato. Watendaji wa kibinadamu wameshika kiasi cha huduma na majibu yao ili kutimiza mahitaji ya dharura, lakini maendeleo yanayohusiana na janga kama vile kuongezeka kwa udijitali kwa kiasi pia kuzuia wakimbizi na watafuta hifadhi kupata huduma.

Majibu yanaonyesha kwamba licha ya kutofautiana kwa changamoto kukabiliwa nazo, **wakimbizi wenyewe na mashirika yanayoongozwa na wakimbizi yana jukumu kubwa katika kukabiliana na janga.** Wanatenda kama wawasilishaji katika hatari zinazohusiana na COVID-19, kama waelimishaji wa usafi na hatua za usalama, na kama watoa rasilimali za vifaa kama vile masks za uso au sabuni pamoja na msaada wa kisaikolojia na kijamii.

Katika kiwango kikubwa cha kijamii data inaonyesha kwamba **janga limepelekea uwepo wa mvutano kati ya wakimbizi na jumuiya za kuwapokea**, hasa kuhusu kupata rasilimali. Zaidi yake, wakimbizi wanakabiliwa na mitazamo ya chuki dhidi ya nchi kadhaa kwa kulaumiwa kuleta virusi. Hata hivyo, washiriki pia waliangazia **mazoea yaliyofanywa na wakimbizi na mashirika ya misaada wakati wa janga hilo ili kupunguza mvutano na kuchangia katika hali ya amani.**

Utafiti huu wa ubora hauonyeshi tu athari nguma za janga hili bali pia mazoea mbalimbali ya kitaifa na ya ndani ili kukabiliana na janga hili. Matokeo yanaonyesha kwamba **majibu ya COVID-19 katika nyanja zote lazima kuzingatia makundi hatarishi**, ikiwa ni pamoja na wakimbizi na watafuta hifadhi, kuchukua tahadhari za kutosha za mahitaji yao na kuzingatia usalama wao.

Utafiti huu ulifanyika kama sehemu ya miradi ya utafiti "Uhamiaji wa lazima, Wanawake – na Amani? Mazoea ya kujenga amani ya wanawake katika kambi za wakimbizi" (DSF and [Osnabrück University](#)) na "Uhamisho wa lazima ndani ya Afrika: Siasa na wadau wa utawala wa uhamiaji" (DSF and [Arnold Bergstraesser Institute](#)). Miradi hiyo inafadhiliwa kwa kujitegemea na Foundation ya Ujerumani ya Utafiti wa Amani (German Foundation for Peace Research, DSF). Kutokana na janga hilo, wachunguzi wakuu wa miradi hiyo waliamua kushirikiana na kuunganisha kujifunza kwa pamoja katika mtazamo wa kulinganisha athari za janga hilo kwa wakimbizi na ulinzi wa wakimbizi.

Nadine Segadlo, Ulrike Krause, Franzisca Zanker, Hannah Edler

12 | 2021